

# **Fasihi Tafsiiriwa za Kigeni: Urafiki au Uadui kwa Fasihi ya Kiswahili**

Joseph Nyehita Maitaria; Peter M. Kinyanjui na Leah Mwangi

## **Ikisiri**

Makala haya yanafafanua mustakabali wa fasihi tafsiiriwa za kigeni kwa fasihi ya Kiswahili. Kupitia tafsiiri, fasihi hizo za kigeni zimekuwapo Afrika Mashariki wakati wa ukoloni na hata baada ya ukoloni. Katika enzi ya ukoloni na hasa katika miaka ya 1930, uhaba wa vitabu vya kufundishia Kiswahili na fasihi yake ulijitokeza. Vitabu hivyo vilihitajika kwa dharura ili kuitikia wito wa serikali ya ukoloni ya wakati huo. Kutokana na sera ya serikali ya ukoloni kuhusu lugha, kuliundwa Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki (ILC). Vitabu vichache vya lugha na fasihi vilikuwapo. Watunzi wachache wenyeji pia walijitokeza kuchangia wito huo. Harakati za kutafsiiri kazi za fasihi za kigeni nazo ziliendelea hata baada ya mataifa hayo ya Afrika Mashariki kupata uhuru. Swali hapa ni: Kuna haja ya kuendelea kutafsiiri fasihi za kigeni kwa Kiswahili? Fasihi tafsiiriwa hizo za kigeni zina athari gani kwa fasihi ya Kiswahili? Katika muktadha huu, makala haya yanatathmini nafasi ya fasihi hizo na athari yake kwa fasihi ya Kiswahili. Kadhalika, makala haya yanapendekeza namna fasihi tafsiiriwa za kigeni zinavyoweza kuichangia fasihi ya Kiswahili katika uwasilishaji na uhifadhi wa utamaduni wa wenyeji wa Afrika Mashariki.

## **1.0 Utangulizi**

Kabla ya uhuru katika mataifa ya Afrika Mashariki hasa katika enzi ya ukoloni, kulikuwa na vitabu vichache mno vya fasihi andishi ya Kiswahili. Katika kipindi hicho, serikali ya kikoloni ilihitaji vitabu vya kufundishia lugha na fasihi kwa Kiswahili. Kwa kuitikia wito huo, Kamati ya Lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki (ILC) iliundwa mwaka wa 1930. Baadhi ya tungo za ushairi wa Kiswahili zilizokuwapo kabla na baada ya utawala wa kikoloni kukiwa Afrika Mashariki ni kama vile *Mashairi ya Muyaka bin Hajji*, *Mwana Kupona*, *Utenzi wa Al Inkishafi* na *Mashairi ya Fumo Lyongo*. Kadhalika, fasihi tafsiiriwa chache za kigeni zilizokuwapo katika miaka ya kabla 1930 ni kama vile: *Alfu-Lela-Ulela*, *Hadithi za Esopo*, *Kisiwa Chenye Hazina* na *Hekaya za Abunuwasi*. Fasihi tafsiiriwa za awali ziliwasilisha maudhui ya kiburudani na mafunzo ya kimaadili. Shughuli ya kutafsiiri iliendelezwa zaidi kwa himizo la serikali ya ukoloni kupitia sera ya lugha ya wakati huo. Kutokana na sera hiyo, kuliundwa

Kamati ya Lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki (ILC). Ingawa hatua hiyo ilikuwa ya serikali ya ukoloni; hilo lilikuwa ni tukio muhimu la kihistoria katika maendeleo ya fasihi na lugha ya Kiswahili. Kulingana na Mbaabu (1996: 68), mojawapo ya malengo ya Kamati hiyo ilikuwa ni kupanga mkakati wa kuhakikisha kuwa vitabu vya Kiswahili vinapatikana ili kuweza kutumika katika taasisi za elimu kote Afrika Mashariki.

Kutokana na wito wa Kamati ya Lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki (ILC), baadhi ya wenyeji wenye vipawa vya utunzi kama vile Shaaban Robert, walijitokeza. Katika kipindi cha sasa, fasihi ya Kiswahili imestawi si haba na harakati za kutafsiri fasihi za kigeni kwa Kiswahili bado zinaendelea (Ruhumbika, 1983). Swali ni: Je, fasihi tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili zilizo bora ni zipi? Je, katika kipindi cha sasa kuna haja ya kuendelea kuibugiza fasihi ya Kiswahili fasihi tafsiriwa za kigeni? Fasihi tafsiriwa za kigeni zina athari gani katika fasihi ya Kiswahili? Katika muktadha huu, ni muhimu kufahamu kuwa kuna 'tafsiri bora' na pia kuna 'bora tafsiri.' Kadhalika, fasihi tafsiriwa kwa Kiswahili zina athari gani za kitamaduni kwa umma wa Afrika Mashariki unaotumia zaidi lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao ya kila siku?

## 2.0 Kazi za Fasihi Tafsiriwa za Kigeni kwa Kiswahili

Katika miaka ya 1930 kazi za fasihi za kigeni<sup>1</sup> zilizotafsiriwa kwa Kiswahili zilikuwa chache mno. Kazi hizo zilitokana na lugha za mataifa ya Ulaya na Asia. Baada ya uhuru kupatikana katika miaka ya 1960 hadi sasa, fasihi za kigeni zinaendelea kutafsiriwa kwa Kiswahili. Miongoni mwa fasihi hizo za kigeni zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ni: *Oedipus The King* 'Mfalme Edipode' (Sophocles), *Antigone* 'Antigoni' (Sophocles), *Merchant of Venice* 'Mabepari wa Venisi' (W. Shakespeare), *The Government Inspector* 'Mkaguzi Mkuu wa Serikali' (N. Gogol) na *Animal Farm* 'Shamba la Wanyama' (G. Orwell). Katika msururu huo kuna zile zilizotungwa kwa lugha za kigeni kwa kuzingatia utamaduni na mazingira ya wenyeji wa Afrika. Miongoni mwa kazi hizo za fasihi ni: *Things Fall Apart* 'Shujaa Okonkwo' (Achebe, 1958), *The Trials of Brother Jero* 'Masaibu ya Ndugu Jero' (Soyinka, 1963), *Arrow of God* 'Mshale wa Mungu' (Achebe, 1964), *The Black Hermit* 'Mtawa Mweusi' (Ngugi, 1968), *A Man of the People* 'Mwakilishi wa Watu' (Achebe, 1968), *Dying in the Sun* 'Kivuli Kinaishi' (Palangyo, 1968), *The Beautiful Ones Are*

---

<sup>1</sup> Hizi ni kazi asili za fasihi ambazo zimewasilishwa kwa lugha za Ulaya na Asia: Kiingereza, Kifaransa, Kirusi, Kiyunani na Kiarabu. Pia, kazi hizo zinaweza kuwa zinatoka katika mataifa ya Afrika au nje ya Afrika. Kazi zilizotafsiriwa kutoka Kiswahili kwenda lugha nyingine hazikuzingatiwa katika makala haya.

*Not Yet Born* ‘Wema Hawajazaliwa’ (Armah, 1969), *The Burdens* ‘Mizigo’ (Ruganda, 1972), *Betrayal in the City* ‘Usaliti Mjini’ (Imbuga, 1976) na *The Trials of Dedan Kimathi* ‘Mzalendo Kimathi’ (Ngugi na Mugo, 1972)

Kwa maoni yetu, fasihi za kigeni zilizotafsiriwa kwa Kiswahili (hasa zile za kutoka Ulaya), zina nafasi finyu katika muktadha wa utamaduni wa wenyeji wa Afrika Mashariki. Hii inatokana na sababu kwamba, kazi hizo zimezingatia mazingira na utamaduni wa kigeni na ujumbe unaowasilishwa hufasiriwa kwa mitazamo hiyo. Maandiko yanayotokana na mazingira ya Afrika, kwa kiasi fulani, yanakaribiana na utamaduni wa Waswahili katika kauli na maneno yaliyotumika na kwa kuzingatia uwasilishaji wa ujumbe. Hii ni kwa kuwa kazi hizo zimezingatia tamaduni za wenyeji wa Afrika. Kimsingi, kuna uwiano mkubwa wa kimaono na wa kifalsafa katika tamaduni za wenyeji (Maitaria, 2018). Aidha, lugha za kigeni zinazotumika katika kazi hizo ni zile zilizorithiwa kutoka utawala wa kikoloni katika mataifa hayo. Kwa hivyo, lugha hizo za kigeni ni chombo cha uwasilishaji tu (Thiong’o, 1986: 28). Baadhi ya watunzi waliotumia lugha za Ulaya (au za kigeni) wana maoni kuwa, malengo yao yalikuwa kwamba kazi zao ziwe za kimataifa na kufikia hadhira pana. Watunzi hao, wanaweza kuchukuliwa kuwa hawakuziabudu lugha za kigeni bali walizitumia kama chombo cha uwasilishaji tu.

### **2.1 Mfasiri wa Kazi za Fasihi**

Kila utanzu wa fasihi unaotafsiriwa huzingatia taratibu maalumu ili kuuwasilisha ujumbe asili uliokusudiwa kwa mihimili ya lugha inayoeleweka kwa hadhira. Kadhalika, maumbo, mitindo na mafumbo katika tanzu asili zinazohusika sharti yadumishwe au yashabihiane kwa kiwango fulani. Maelezo hayo yanatokana na mawazo ya baadhi ya wataalamu wa tafsiri kama vile: Kinge’i (2017), Jilala (2016), Habibu (2016), Haule na Feslas (2012), Malangwa (2008) na Ruhumbika (1983) na Nida (1964). Kwa kuzingatia mawazo ya wataalamu hao, mfasiri bora wa tanzu za fasihi anatarajiwa:

- i. Awe na kiwango fulani cha kumudu sarufi za lugha zote mbili zinazohusishwa katika uwasilishaji wa kazi husika za fasihi;
- ii. Awe na utambuzi wa kutosha kuhusu utamaduni wa lugha asili na lugha pokezi. Kwa kuzingatia hili mfasiri ataweza kuuwasilisha ujumbe kwa namna inayokubaliwa katika muktadha wa lugha lengwa;
- iii. Awe na ujuzi wa kutosha kuhusu utumiaji wa kamusi na marejeleo mengine yanayohusiana na lugha husishwa hizo katika mchakato wa tafsiri. Hii inatokana na sababu kwamba, baadhi ya maneno yaliyotumika katika kazi asili huhitaji ufafanuzi au visawe vya maana. Kwa kufanya hivyo, mfasiri anaweza kubaini maana ya matini

zilizotumika na pia kuepukana na baadhi ya vizingiti vinavyoweza kujitokeza katika shughuli hiyo ya kutafsiri tanzu za fasihi;

- iv. Awe na uwezo wa kuratibu kwa mantiki na kuwasilisha mawazo kwa muwala unaozingatia kaida za sarufi ya lugha asili na lugha lengwa; na,
- v. Awe mwenye subira katika kutenga muda wake ili kuzisoma na kuzifasiri matini nzima anazozingatia kabla ya kuzamia kazi ya kutafsiri. Aidha, anapaswa kuzingatia hayo kwa malengo ya kuelewa ujumbe unaowasilishwa na pia kuteua msamiati sadifu katika uwasilishaji wa tafsiri yake.

Kwa kuzingatia sifa hizo zilizorejelewa hapo juu, tanzu za fasihi tafsiiriwa zitakuwa za kiwango cha kukubalika, na mchakato wa kuzifasiri utakuwa na urahisi usiotatiza. Kadhalika, upotoshaji wa maana utadhibitiwa kwa kiwango fulani katika lugha pokezi.

### **2.3 Changamoto katika Fasihi Tafsiiriwa za Kigeni katika Kiswahili**

Katika mataifa ya Afrika Mashariki, kichocheo cha fasihi tafsiiriwa za kigeni kwa sasa ni bayana. Kwa mfano, kazi za fasihi tafsiiriwa zinazotokana na mataifa ya kigeni bado zinahitajika ili kuchangia hazina ndogo iliyopo katika tafiti na tahakiki za taaluma ya fasihi linganishi (Jilala, 2016: 10; Ponera, 2014: 49). Baadhi ya wataalamu wa tafsiiri wameeleza kuwa matini za fasihi hutatiza mno zinapolinganishwa na matini nyingine (Nord, 2005). Aidha, vitabu hivyo vinahitajika kukidhi haja za wasomaji wa lugha ya Kiswahili. Mapitio ya fasihi za kigeni zilizotafsiiriwa yanabainisha changamoto mbalimbali za kiufasiri. Mathalani, baadhi ya dhana muhimu zimewasilishwa kwa kuipotosha hadhira. Suala hili linaweza kubainika kwa kuzingatia tafsiiri za anwani za vitabu. Katika *Things Fall Apart* 'Shujaa Okonkwo' (Achebe, 1958) - anwani katika riwaya asili inahusu mambo ambayo hayakuwa kama ilivyotarajiwa. Anwani iliyopo ni ya mhusika mkuu anayechukiliwa kuwa shujaa. Mwelekeo huo pia unapatikana katika tafsiiri ya anwani ya *Othello* 'Othello - Tanzania ya Mtu Mweusi' (Mukwana, 2015) - anwani ya tamthilia asili imetafisiiriwa kimuktadha kwa kuzingatia maudhui. Katika *The Beautiful Ones Are Not Yet Born* 'Wema Hawajazaliwa' (Amah, 1969) - mfasiri amefasiri anwani ya 'The Beautiful Ones...' - kuashiria 'utu' au 'wema'. Uelekeo huo unatokana na yaliyomo ndani ya riwaya (hii si tafsiiri ya moja kwa moja bali mfasiri alijipa uhuru katika kuwasilisha hoja na kuondoa utata unaoweza kujitokeza endapo angezingatia maana za maneno ya 'Beautiful...' yaani 'Waremba' au 'Wazuri.'). Isitoshe,

baadhi ya masuala yaliyojadiliwa katika riwaya hiyo yanaweza kueleweka kwa kurejelea muktadha wa kihistoria katika taifa la Ghana katika miaka ya mwishoni mwa 1960 na mwanzoni mwa 1970 (Kinge'i, 2017). Changamoto nyingine inayoweza kujitokeza ni pale mfasiri wa Kiswahili anapokumbana na 'tafsiri ya tafsi'ya fasihi ya kigeni (Adungo, 2015). Mfano wa tafsi hiyo ni tamthilia ya *Sophocles* (awali lugha iliyotumika ilikuwa ni ya Kiyunani na baadaye kutafsiwa kwa lugha nyinginezo kama vile Kiingereza na mwishowe kutafsiwa kwa Kiswahili).

Katika muktadha wa tafsi za kigeni zilizopo hapo juu, kuna baadhi ya maswali ambayo yanahitaji majibu, kwa mfano, fasihi tafsiwa kwa Kiswahili zilikuwa na dhima gani katika jamii za Afrika Mashariki kabla ya uhuru? Kwa kipindi cha sasa fasihi tafsiwa kwa Kiswahili zina mchango gani katika fasihi ya Kiswahili? Hapa kuna haja ya kufahamu dhima ya fasihi tafsiwa za kigeni na athari zake kwa hadhira ya fasihi ya Kiswahili kwa jumla. Dhana ya tafsi imefasiwa kama njia ya uhamishaji wa mawazo na maana (katika lugha andishi) kutoka lugha asili hadi lugha pokezi (Mwansoko, 1996: 43; Catford, 1965: 20). Kwa hivyo, tafsi ni shughuli ya uhamishaji wa maana, mawazo, dhana au ujumbe uliowasilishwa kwa maandishi kutoka lugha asili na kuvika visawe vyake kwa kuzingatia lugha lengwa. Kadhalika, Landers, (2001) ameeleza kuwa, tafsi ambazo si sisizi huwa na kiasi fulani cha ugumu katika kufahamu ujumbe unaowasilishwa. Kwa kuzingatia fasihi tafsiwa za kigeni kwa Kiswahili, inabainika kuwa kazi hiyo inapokamilika huwa ni tunda la kongamano la tamaduni mbili au zaidi.

Awali katika makala haya, tumefafanua baadhi ya sifa ambazo mfasiri anapaswa kuzingatia kabla ya zoezi la kutafsi kazi za kigeni kwa Kiswahili. Mchakato wa kutafsi na kufasi matini za fasihi si jambo jepesi; linahitaji uzoefu wa kutathmini maneno na kauli zilizotumika kupitia jicho la utamaduni lengwa. Kwa msingi huu kuna ubunifu wa kiwango fulani katika uwasilishaji wa maana na ujumbe asili kwa lugha pokezi. Kadhalika, kazi za fasihi tafsiwa ni tofauti na zile asili. Zaidi ya ubunifu, fasihi tafsiwa zinahitaji kukitwa kwenye mshabaha wa ujumbe na maana inayowasilishwa (Shulte na Gerhard, 1993: 86). Sababu ni kwamba, mawazo yanayowasilishwa kwenye fasihi tafsiwa za kigeni huwa na tabia ya kujikita kwenye mwelekeo wa mfasiri. Hizo ni changamoto zinazoweza kukabiliwa kabla ya zoezi la fasihi tafsiwa kukamilika na kuwasilishwa kwa hadhira. Baadhi ya changamoto hizo zinadokezwa hapa:

- i. Kuwa, tafsi ya kifasihi si sisizi (yaani si ya moja kwa moja). Kuna haja ya kupitia makala nzima na kubaini miundo ya sentensi, maneno na vishazi katika matini ya fasihi asili. Hii inamaanisha kuwa, ruwaza za maneno zikichukuliwa kijuujuu na kutafsiwa kwa jitihada ya kujifunga

zaidi katika miundo hiyo, ujumbe unaweza ukapotoshwa. Kwa kuzingatia aina hii ya tafsiri huenda ujumbe ukawa unawasilishwa bila ya kuzingatia matakwa ya kisarufi katika lugha pokezi. Aidha, tatizo hili huchangiwa zaidi na tofauti za kitamaduni na ukosefu wa msamiati sadifu ambapo neno moja huweza kuwa na maana zaidi ya moja (Wanjala, 2002: 13). Mfasiri mwenye uzoefu hung'amua kuwa kuna umuhimu wa kuzingatia hayo ambayo ni hatua ya awali katika mchakato wa uwasilishaji wa ujumbe unaotarajiwa;

- ii. Kuwa, tathmini ya fasihi tafsiriwa inaweza kufanyika kabla ya kuanza mchakato wa tafsiri, katikati au mwishoni mwa shughuli hii kutegemea aina za matini lengwa (Malangwa, 2008). Aidha, matini hizo mbili (asili na lengwa) zinazotofautiana hutumia taaluma za lugha ambazo hazina uhusiano wa karibu. Kwa hivyo, ni nadra kupata wafasiri wanaomudu lugha husika kwa kiwango kinachohitajika. Kwa sababu hii, tafsiri ni harakati ambayo inaendelea na kuendelezwa zaidi hata baada ya rasimu ya kwanza kukamilika;
- iii. Kuwa, ni vigumu kupata visawe katika lugha lengwa hasa inapozingatiwa kuwa matini asili inaweza kuwa imewasilishwa kwa lugha ya zamani, sajili au lahaja. Katika kukabiliana na tatizo hili, mfasiri anaweza kuwasilisha rasimu yake kwa lugha ya wastani ili kuweza kueleweka na kuuwasilisha ujumbe kwa hadhira pana. Hata hivyo, matokeo ya mbinu hii yanaweza kuifanya tafsiri hiyo kuwa na viwingu vya maana na kupanua zaidi mawanda ya utafsiri wa ujumbe ambapo kuna uwezekanao wa kuupotosha ujumbe asili. Si maana zote zinaweza kukumbatiwa mia kwa mia kutoka kwa lugha ngeni, hata pale lugha za tamaduni mbili zinapotagusana;
- iv. Kuwa, ujumi katika kazi za fasihi hujitokea katika vipengele vya kauli za lugha ambazo si rasmi. Hivyo, kiwango cha ubunifu cha mfasiri hutokana na tajiriba yake na hilo hujitokeza katika uwasilishaji wa kazi yake ambapo pamoja na kwamba tafsiri ni upitishaji wa ujumbe au mawazo, lakini hiyo haitoshi kwa sababu, fasihi tafsiriwa ni kazi ambayo pia imebuniwa kwa kiwango fulani;
- v. Kuwa, matumizi ya tamathali za usemi katika uwasilishaji wa fasihi, humtarajia mfasiri wa fasihi kutafakari zaidi kuhusu namna mwafaka ya kufumbua mafumbo yaliyofumbwa kupitia utamaduni wa lugha asili;

hapa tunaangazia baadhi ya semi ambazo ni viashiria fiche vinavyoweza kueleweka kwa kuzingatia utamaduni wa lugha asili; na,

- vi. Kuwa, baadhi ya maneno yanayotumika katika fasihi tafsiriwa kwa Kiswahili huwa na viwango viwili au zaidi vya kimaana. Kwa mfano, kauli teule katika jamii huweza kutamkwa na kutumiwa kama ishara inayoakisi maana inayokusudiwa katika jamii lugha mahususi. Sababu hapa ni kwamba, watu hutumia lugha kuwasilisha ujumbe kwa mujibu wa malengo yao (Wanjala, 2002: 98). Hivyo, msamiati unaweza kuwa wa kawaida lakini kutokana na namna unavyotumiwa unaweza kuakisi maana inayofungamana na muktadha unaorejelewa katika utanzu asili.

Hoja hizo hapo juu zinabainisha kuwa fasihi tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili huweza kudumisha au kudhoofisha kiwango cha lugha na ujumbe unaowasilishwa. Hii inatokana na uhuru alionao mfasiri katika kuteua maneno sadifu katika muktadha wa utamaduni pokezi. Kadhalika, fasihi hizo tafsiriwa haziwezi kuwa kamilifu kwa sababu zina viwingu vitokanavyo na wale wanaotafsiri. Iwapo ujumbe utakuwa hausadifu utamaduni wa wenyeji aghalabu hudondoshwa au kuwasilishwa kwa ujumla. Endapo mfasiri atajitahidi kudumisha miundo ya lugha asili, matokeo yanaweza kuathiri upokezi wa hadhira ya fasihi ya Kiswahili. Katika muktadha huu, kuna haja ya kutathmini athari zinazoweza kujitokeza bila ya mfasiri kukusudia. Swali hapa ni: fasihi tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili zimeathiri kwa kiwango gani fasihi ya Kiswahili? Je, kuna uwezekano wa kuzikumbatia fasihi tafsiriwa za kigeni (na hasa zile kigeni zinazotokana na utamaduni wa nje ya bara la Afrika)? Katika muktadha unaorejelewa hapa ni kuwa, fasihi tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili zinaweza kuwa adui au rafiki wa fasihi ya Kiswahili. Katika sehemu inayofuatia tutaeleza namna sura hizo mbili zinavyojitokeza.

#### **2.4 Fasihi Tafsiriwa za Kigeni katika Fasihi ya Kiswahili**

Kipindi cha sasa hapa Afrika Mashariki kimeshuhudia kazi nyingi za fasihi tafsiriwa kwa Kiswahili (mifano ya kazi hizo imedokezwa hapo awali katika makala haya). Afrika Mashariki ilibarikiwa kupata wageni kutoka mataifa mbalimbali kama vile: Uarabuni, Ujerumani na Uingereza. Katika karne ya 18 wageni kutoka mataifa ya Mashariki ya Kati walikuja kufanya biashara na baadhi ya kazi zao za fasihi ziliweza kutafsiriwa kwa Kiswahili. Wengine waliofika katika maeneo ya Afrika Mashariki ni Wamisionari waliokuwa na malengo ya kueneza Ukristo katika karne ya 19 (Mbaabu, 1996). Miongoni mwa Wamisionari walioshughulikia tafsiri za matini kwa Kiswahili ni L. Krapf, J. Rebmann, W. E. Taylor na E. Steere. Pamoja na kufanya tafsiri, walihubiri na

kueneza Injili kwa lugha ya wenyeji. Hivyo, baadhi ya vifungu vya Biblia viliweza kutafsiriwa kwa Kiswahili (Maitaria na Momanyi, 2016). Katika enzi za ukoloni na hasa wakati wa utawala wa Waingereza, tanzu mbalimbali za fasihi za kigeni zilitafsiriwa na kuingia katika fasihi ya Kiswahili (mifano ya tafasiri hizo inapatikana mwanzoni mwa makala haya). Baada ya mataifa ya Afrika kupata uhuru, harakati za kutafsiri fasihi za kigeni zinaendelea kwa kasi. Fasihi tafsiriwa za kigeni zinaweza kuwa na chembe za urafiki au uadui katika fasihi ya Kiswahili kama ifuatavyo:

#### **2.4.1 Urafiki**

Kichocheo cha kutafsiriwa fasihi za kigeni kwa Kiswahili katika Afrika Mashariki katika enzi ya ukoloni na punde baada ya uhuru kilikuwa bayana. Vitabu vya fasihi ya Kiswahili vilikuwa vichache katika miaka ya kabla ya 1960 hadi miaka ya mwanzoni mwa 1980. Hii ilikuwa sababu ya msingi katika miaka hiyo. Kadhalika, kuanzia miaka ya 1980 hadi sasa kuna uhitaji wa vitabu vya fasihi tafsiriwa za kigeni siyo tu katika masuala ya elimu bali pia kukidhi usomaji wa jumla kwa wapenzi wa fasihi kupitia lugha ya Kiswahili. Kwa namna ambavyo shughuli za tafsiri huhitaji umahiri wa lugha na ufasiri wa ujumbe unaowasilishwa; matokeo ni kwamba, mfasiri hujijengea maarifa ya kuwasiliana na hadhira. Kiwango hicho cha ujuzi hupokezwa na mfasiri kupitia mitindo ya lugha iliyotumiwa na mtunzi asili. Kupitia katika mchakato huo wa tafsiri, mfasiri hunoa kunga za uwasilishaji wa fasihi. Hadhira nayo hupitishiwa na kufurahia maarifa hayo, na pia hudadisi zaidi kuhusu masuala ya lugha na maudhui yanayowasilishwa. Sababu ni kwamba, muktadha asili hurejelewa katika uchanganuzi-elekezi kuhusu tamaduni zinazohusishwa (asili na pokezi). Utamaduni asili huzingatwa kwa namna unavyowasilishwa katika muktadha wa utamaduni pokezi. Katika enzi hizi za utandawazi, masuala ya kijamii yanayohitaji kurejelewa ni yale yanayovuka mipaka ya kijamii na kitaifa na kuzingatia mtazamo mpana wa kimataifa. Kwa hivi sasa, Afrika Mashariki si kisiwa na wala haijitengi na maeneo mengine ulimwenguni, linalotokea eneo la Afrika Mashariki linaweza kuwa limeshuhudiwa kwingineko.

Kupitia fasihi tafsiriwa za kigeni, hadhira inaweza kujifunza kwa urahisi kuhusu yale yanayotokea katika sehemu nyingine ulimwenguni. Katika muktadha huu, watu wanaotokana na tamaduni tofauti wanaweza kustahiana na kuvumiliana ili kuimarisha maelewano katika ngazi ya kimataifa. Hivyo, fasihi hii tafsiriwa kwa Kiswahili inakuwa ni ufunguo wa kujenga daraja la ushirika kwa kuzifahamu jamii nyingine. Kwa mantiki hii, viashiria asili vya tamaduni za kigeni hufafanuliwa kwa tajiriba ya wenyeji wa Afrika Mashariki. Fasihi tafsiriwa inaweza kuwa ni chombo cha kuanzisha na kudumisha mahusiano ya



kitamaduni, umoja na utamangamano miongoni mwa wanajamii wanaotokana na jamii au mataifa tofautitofauti ulimwenguni (Maitaria, 2016 na Mutui, 2009). Umataifa huu utatokana na mtagusano wa watu kupitia fasihi tafsiriwa kwa Kiswahili. Kutokana na uhalisi huu, wenyeji wanaweza kujinasua kutokana na ‘ufinyu’ wa mawazo kuhusu mwonoulimwengu wao. Hapa ieleweke kuwa, kila uchao kuna mabadiliko ya kijamii yanayotokana na sayansi na teknolojia ambayo huathiri fikra na mkondo wa maisha ya watu. Mabadiliko hayo yanapojiri, yanahitaji kufafanuliwa kupitia katika upenu wa tanzu za fasihi tafsiriwa. Hivyo, hadhira ya fasihi ya Kiswahili haijaachwa nyuma katika ukumbatiaji wa mawimbi ya mabadiliko yanayoshuhudiwa katika ulimwengu wa sasa. Aidha, katika kujihusisha na shughuli za kutafsiri kazi za fasihi kutoka lugha ya kigeni, mfasiri wa fasihi hizo za kigeni huwa anajijengea mtaji wa kifedha na wa kujiajiri. Kwa maana hii, jitihada hizo binafsi zina tija na zinaweza kuwa ni njia mojawapo ya ajira katika ulimwengu wa sasa ambapo ajira ni adimu. Hata hivyo, baadhi ya wafasiri wana mawazo kuwa wamejitosa katika shughuli ya kutafsiri baadhi ya kazi za fasihi za kigeni kama njia ya kujiburudisha (Landers, 2001). Hiyo inaweza kuwa ni sababu mojawapo na vilevile wafasiri hao hujipatia fedha kutokana na kazi yao. Kadhalika, wataalamu na walimu wa ngazi za juu za kiusomi kama vile wahadhiri wa vyuo vikuu kupitia tafsiri huimarisha nafasi zao katika kupandishwa vyeo kazini. Kupitia fasihi tafsiriwa, watu wa nchi mbalimbali wanaweza kupashana na kusambaziana habari, maana dunia sasa ni kama kijiji kutokana na utandawazi unaowafanya watu kuingiliana kifikra, kitamaduni kisayansi na kiteknolojia.

Kwa mujibu wa Ruhumbika (1983), tafsiri za fasihi za kigeni ni njia mojawapo ya kuikuza fasihi ya Kiswahili. Hivyo, fasihi tafsiriwa husaidia katika kuinua kiwango cha ubora katika uwasilishaji wa fasihi ya Kiswahili. Aidha, tafsiri hizo zinakuwa ni nyenzo za kujifunza lugha ya kigeni na kujifunza miundo na maumbo ya lugha nyinginezo za kigeni. Kwa wafasiri wa fasihi, inakuwa ni njia mojawapo katika kuupanua msamiati. Wanaotafiti lugha na utamaduni wa jamii ngeni huweza kuanzia katika fasihi tafsiriwa na baadaye kulinganisha na fasihi asili ili kuimarisha kiwango chao cha mawasiliano na wenyeji.

#### **2.4.2 Uadui**

Tumeeleza hapo juu kuwa fasihi tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili huweza kuwasaidia wenyeji wa Afrika Mashariki kupanua mawazo kuhusu namna ya kushughulikia migogoro na masuala muhimu kuhusu maisha yao kwa ujumla. Hata hivyo, kuna haja ya kuwa makini katika kukabiliana na fasihi hizo za kigeni zilizotafsiriwa kwa Kiswahili. Swali hapa ni: Je, fasihi tafsiriwa kwa Kiswahili zinahitaji kuchukuliwa kuwa njia ya kuimarisha fasihi ya Kiswahili?

Kwa ujumla, fasihi hizo zina athari gani kwa fasihi ya Kiswahili? Maswali hayo yanaangaziwa hapa kwa malengo ya kufafanua yale yasiyofaa katika muktadha wa fasihi ya Kiswahili. Hapa ieleweke kuwa, tafsiri ni shughuli ya uhamishaji wa mawazo yaliyopo kwenye maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Ujumbe katika fasihi tafsiriwa huwasilishwa katika mazingira ya kigeni yasiyokuwa na mshabaha mkubwa na mazingira ya asili ya Afrika. Ingawa kwa kiasi fulani ujumbe unaweza kuwa uleule; ujumbe huo huwa umeshughulikiwa na kuwasilishwa katika muktadha wa kigeni. Hivyo, tafsiri hizo za fasihi ya kigeni ni vyombo vinavyobeba mawazo yaliyojikita katika muktadha yenye asili ya kigeni.

Kulingana na Tugarara (2013) ni kwamba, Kiswahili kinapodharauliwa kwa kupendelea lugha ya kigeni, hususani Kiingereza, tutakuwa tunakidharau chetu na kukitukuza cha wengine. Aidha, wapokezi wa fasihi hiyo huweza kujengewa mwelekeo (hata bila ya kukusudiwa) kwamba, fasihi zinazobuniwa na kuwasilishwa kwa mazingira ya wenyeji ni za kiwango cha chini au ubora wake ni wa kutiliwa shaka. Kuna uwezekano wa kizazi cha sasa kuiga kimkumbo (na hata bila ya kudadisi) utamaduni wa kigeni kwa kupitia fasihi hizo. Baadhi ya vijana wanaweza kuiga mambo ambayo hayawiani na utamaduni uliowazaa na kuwalea. Utamaduni huo wa kigeni kupitia katika fasihi tafsiriwa huweza kuchukuliwa kuwa ni ‘ustaarabu’ na ‘utamaduni wa maendeleo’ katika jamii. Kwa mantiki hii, fasihi tafsiriwa ni nyenzo inayoweza kutumiwa holela katika uigaji na ujifunzaji wa utamaduni wa kigeni. Fasihi tafsiriwa hazikomei tu kwenye uwasilishaji wa matini bali huingiza chembe fulani ya utamaduni wa lugha zilizohusishwa katika uwasilishaji huo.

Katika muktadha wa hoja hizo zilizowasilishwa hapo juu, inabainika kuwa fasihi tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili huweza kuwa na manufaa na kwa kiasi fulani huweza kujengea fasihi ya Kiswahili mazingira ya ushindani wa kimwelekeo. Ikibidi kuwapo kwa fasihi tafsiriwa kwa Kiswahili ni muhimu kutahadharisha kuwa fasihi ya wenyeji (katika muktadha huu ni fasihi ya Kiswahili) isijengewe mazingira hayo ya ushindani kutoka kwa fasihi za kigeni.

Kwa sasa lugha ya Kiswahili haijatindikiwa katika kushughulikia masuala mbalimbali ya kilimwengu bila ya kujiegemeza katika lugha za kigeni. Iwapo kuna haja ya kuwapo kwa fasihi hizo tafsiriwa kwa Kiswahili katika kushughulikia masuala yanayohusu maisha ya wenyeji wa Afrika Mashariki, ni bora kuangazia kwanza zile zilizochipuka kutokana na mazingira ya Afrika. Endapo pana haja ya kuwa na fasihi linganishi, fasihi zinazotokana na tamaduni za mataifa ya Ulaya, Amerika na Asia, zinaweza kutafsiriwa. Kuwapo kwa fasihi tafsiriwa kunaweza kujenga kasumba miongoni mwa wenyeji kuwa,

fasihi ya Kiswahili haiwezi kujisimamia katika uwasilishaji wa masuala yanayotokana na tajiriba ya wenyeji na hata masuala ya kidhahania.

### **3.0 Hitimisho**

Kupitia fasihi tafsiriwa ya kigeni katika Kiswahili, wenyeji wa Afrika Mashariki wana chombo cha kuwajumuisha na kujenga maelewano ya 'kimataifa'. Kwa kuzingatia mwelekeo huu tofauti za kitamaduni au kitaifa zitapunguzwa. Kimsingi, hadhira ya fasihi ya Kiswahili hujitambulisha zaidi kwa kujiegemeza katika utamaduni mmoja unaoshirikisha jamii mbalimbali zilizopo Afrika Mashariki. Katika makala haya yamependekezwa namna fasihi tafsiriwa za kigeni zinavyoweza kuujenga utangamano wa wenyeji wa Afrika Mashariki kama jamii. Sababu ni kwamba, zaidi ya fasihi kuwa ni chombo cha burudani; huhifadhi na huelimisha kuhusu utamaduni husika. Hii ni pamoja na fasihi za kigeni zilizotafsiriwa kwa Kiswahili. Lugha ya Kiswahili inayotumika katika mchakato wa uwasilishaji wa fasihi za kigeni huwa ni chombo tu ambamo tamaduni za kigeni husetiriwa. Kutokana na mazingira haya, kuna haja ya kuzichuja fasihi hizo ili zisiwe chombo cha kuukaribisha ukoloni mamboleo kupitia mlango wa nyuma. Zaidi ya kujiegemeza katika fasihi hizo tafsiriwa, kuna haja ya kuimarisha fasihi za wenyeji kwa lugha ya Kiswahili. Kwa njia hii, wenyeji wa Afrika Mashariki watakuwa wanaulea zaidi utamaduni wa Kiafrika. Mwafaka huo utakapofikiwa ndipo jamii za Afrika zitakuwa zimejikomboa kikamilifu kutokana na minyororo ya ukoloni mkongwe na ukoloni mamboleo. Jambo la kujiuliza hapa ni kwamba: Fasihi hizo za kigeni zinapopenyenzwa katika mazingira ya Afrika kupitia tafsiri, vijana watakuwa wanajengewa mwelekeo gani katika maisha yao? Suluhu hapa ni kuendeleza na kuudumisha utamaduni wa asili kwa kutunga na kuwasilisha kazi za fasihi kwa lugha ya wenyeji wa Afrika ambapo lugha hiyo ni Kiswahili. Iwapo kuna haja ya kushirikisha fasihi tafsiriwa za kigeni katika uga wa fasihi ya Kiswahili, ziwe ni zile zinazoakisi utamaduni wa wenyeji. Fasihi ya wenyeji wa Afrika Mashariki isipostawishwa kwa Kiswahili itakuwa ni kujitanda ngozi ya Uafrika ilhali ndani yetu tutakuwa ni wageni. Isitoshe, kuendelea kuzitafsiri zaidi fasihi za kigeni itakuwa ni kujidhalilisha kwa wageni, na utamaduni wa wenyeji utakuwa unagezwa kwa mizani zenye asili ya kigeni.

## **Marejeleo**

- Adungo, C. (2015). “Uhusiano wa Tafsiiri na Taaluma Nyinginezo” katika ‘Ukumbi wa Lugha na Fasihi’ katika *Taifa Leo*, Tarehe 28.8. 2015. Nation Media Group Ltd. uk. 26.
- Bakize, L.H. (2013). *Tafsiiri na Ukalimani*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.
- Habibu, N. (2016). “Tafsiiri katika Tamthiliya ya Kuigizwa” katika Jilala, H. (Mhar.) *Nadharia za Tafsiiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company Ltd. kur. 294-307.
- Haule, F.C. na Feslas, T.K. (2012). *Nadharia ya Ukalimani: Sekondari na Vyuu*. Songea: Peramiho Printing Press.
- Jilala, H. (2016). “Uhakiki wa Nadharia ya Scopos katika Tafsiiri: Mifano ya Tafsiiri ya Matini za Kiutamaduni” katika Jilala, H. (Mhar.) *Nadharia za Tafsiiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company Ltd. kur. 70-91.
- Kinge’i, K. (2017), “Challenges of Translating Creative Literature from English into Kiswahili” katika *Mwanga wa Lugha Juz.1 Na. 2*. Eldoret: Moi University Press, kur. 43-54.
- Landers, C.E. (2001). *Literary Translation: A Practical Guide*. Toronto: Multilingual Matters Ltd.
- Maitaria, J.N. (2018). “Methali kama Kitambulisho cha Utamaduni wa Mwafrika” katika Ndungo, C. na wenzake (Wah.) *From Asmara 2000 to Nairobi 2014: Trends in African Languages and Literature*. Nairobi: Institute of African Studies, Kenyatta University kur. 406-419.
- Maitaria, J.N. na Momanyi, C. (2016). “Visawe katika Methali Tafsiiriwa za Kiswahili” katika Jilala, H. (Mhar.) *Nadharia za Tafsiiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company Ltd. kur. 275-293.
- Malangwa, P.S. (2008). “Ukiushi katika Kufasiri Matini za Kiswahili: Mifano kutoka Tafsiiri ya Julius Kambarage Nyerere: *Mabepari wa Venisi*” katika *Kiswahili*, Dar es Salaam: TUKI, Juz. 71, kur. 24-33.
- Mbaabu, I. (1996). *Language Policy in East Africa*. Nairobi: Educational Research and Publication.
- Mutui, J.A. (2009). “The Adequacy of Translation Theory with Respect to Drama: The Case of Samwel Mushi’s *Mfalme Edipode*.” *Tasnifu ya Uzamili* (Haijchapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- Mwansoko, H.J.M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation*. London: Prentice Hall.
- Nida, E. (1964). *Towards a Science of Translation with Special Reference and Procedures in Bible Translating*. Leiden: E.J. Brill.
- Nord, C. (2005). *Text Analysis in Translation: Theory, Methodology and Didactic Application*. New Jersey: Rodopi.
- Ponera, A.S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.
- Ruhumbika, G. (1983). "Tafsiri za Kigeni katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili" katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI, kur. 253- 266.
- Shulte, H. na Gerhard, T. (1993). *The Art of Literary Translation*. London: University Press of America.
- Thiong'o, N. (1986). *Decolonising the Mind: the Politics of Language in African Literature*. Nairobi: Hienemann Educational Books Ltd.
- Wanjala, F.S. (2002). *Misingi ya Ukalimani na Tafsiri kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Bookshop.

